
# Dawa ya Maambukizo Fiche ya TB Rifampin (RIF)

TB FREE
KING COUNTY

Utakunywa dawa yako mara moja kwa siku kwa miezi 4.

Utameza vidonge vyako vya kila siku pamoja kwa wakati mmoja.

Waambie madaktari wako wengine kwamba unatumia dawa ya TB isiyo amilifu.



Una maambukizo fiche ya TB, aina ya maambukizo ya TB. Huna ugonjwa wa TB na huwezi kueneza TB kwa watu wengine. Dawa hii itasaidia kuzuia ugonjwa wa TB amilifu.

| Dawa | Idadi ya vidonge kwa siku |
|---|---|
| Rifampin | |



**Nitakunywa dawa yangu kila siku kwa miezi 4**

Piga simu muuguzi wako ikiwa una maswali au madhara:

______________

Public Health
Seattle & King County




TB FREE
KING COUNTY

ACHA kutumia dawa zako mara moja na UPIGIE SIMU muuguzi wako wa TB ikiwa una matatizo yoyote kati ya yafuatayo:

- Hamu kidogo au hakuna hamu ya chakula
- Kuumwa kwa tumbo au mkakamao wa misuli ya tumbo
- Kichefuchefu ama kutapika
- Mkojo wa rangi ya kola au vinyesi vyepesi
- Ngozi au macho ya manjano
- Kuchibuka au kutokwa na damu kwa urahisi
- Upele au kuwashwa
- Udhaifu mkubwa au uchovu
- Homa
- Maumivu ya kichwa ama mwili
- Kizunguzungu
- Kuwashwa au kufa ganzi katika mikono au miguu yako

**KUMBUKA: Ni sawa ikiwa mkojo, mate, au machozi yako yanageuka rangi ya chungwa. Lenzi laini za mgusano zinaweza kuwa na madoa.**

## Vidokezo vya kutumia RIF

- Weka king'ora ili kukukumbusha kunywa dawa yako
- Meza dawa kwenye tumbo tupu kabla ya kukula chochote
- Ongea na daktari wako ikiwa unakuywa pombe, pombe inaweza kusababisha madhara
- Mwambie daktari wako kuhusu dawa nyingine ambazo unatumia
- Mwulize muuguzi wako ikiwa una maswali

Public Health
Seattle & King County